

Farouk Muslim
1976
MBIO ZA SAKAFUNI
Nairobi: East African Publishing House

Nacherzählt von
Lourenco Noronha
Lektor (1974-2009) für Swahili-Literatur
am
Institut für Afrikawissenschaften der Universität Wien
Taasisi ya Taaluma ya Bara la Afrika
Chuo Kikuu cha Vienna

Stand: Mai 2009

Widmung
Kutabaruku

al-hamdu li-llahi
subhanahu wa-ta'ala

Dibaji
Vorwort

Angeregt wurden diese didaktischen Unterlagen von Studierenden am Institut für Afrikawissenschaften der Universität Wien.

Die deutschsprachigen Teile wurden von Dr. Franz Rader korrigiert; dieser hat während seiner Tätigkeit an der Österreichischen Botschaft in Nairobi meine Berufung nach Wien gefördert. Für beides bin ich ihm dankbar.

Lourenco Noronha
E-mail: noronha@gmx.at

1. Einleitung *Utangulizi*

1.1. Biographische Notizen *Wasifu wa Mtunzi*

*Farouk A. Muslim ni kijana mwanasheria, naye ni mdarisi katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Alipata elimu yake katika Alliance High School, Kikuyu, na shahada yake ya kwanza ya sheria L.L.B. katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania, mnamo mwaka 1973. Shahada yake ya pili ya sheria L.L.M. aliipata katika Chuo Kikuu cha Nairobi.*¹

1.2. Thematische Einführung *Kiini (dhamira, dhana, mada, wanda/ma-) maalum*

Das Theaterstück Mbio za Sakafuni gehört zu den Erziehungstexten der 70er und 80er Jahre des vergangenen Jahrhunderts, wie Huka, Salome, Shida, und Sitaki, die auf dieser Website www.swahili-literatur.at in der Reihe Nacherzählungen zu finden sind. Sie sind immer noch aktuell. Dieser Text ist - im Gegensatz zu der damals existierenden Tendenz in Kenia, auf Englisch zu schreiben - auf Kiswahili, in der Sprache der Intellektuellen, aber auch des Volkes verfaßt.

Das Sprichwort *Mbio za Sakafuni huishia Ukingoni* übersetze ich wörtlich mit: „Der schnelle Lauf am Dache endet gewöhnlich am Rand des Daches bzw. man stürzt über ihn in die Tiefe“. Man denkt dabei an ein flaches Dach ohne Zaun am Rande. Die Absicht des Autors lautet: „*Funzo la Farouk Muslim ni kwamba mwanandamu hana budi kuzingatia mawazo ya wenziwe ingawa jukumu la kukata shauri mwishowe humwangukia mwenyewe.*“²

An den beiden weiblichen Personen Halima und Sofia legt der Autor seine Grundthese dar: „Der schnelle Lauf“ bezieht sich auf Halima, die schnell und emotionell handelt. Sophia dagegen ist nüchtern und sachlich. Der Name *Halima* bedeutet eigentlich „geduldig, rücksichtvoll“³. Er paßt nicht zur Person selbst. *Sofia* bedeutet „Weisheit“.

1.3. Literaturhinweise *Marejeo (Marejeleo)*

Die Zahlen in Klammern beziehen sich auf die jeweilige Signatur der Fachbibliothek für Afrikawissenschaften und Orientalistik der Universität Wien.

1.3.1. Primärliteratur

Muslim, Farouk. 1976. Mbio za Sakafuni. Dar es Salaam: EAPH. 49pp. (B.8.9.6.).
Muslim, Farouk/ Mzee, S. 1980. Mkuki wa Moto. Nairobi: EAPH. 59pp. (B.8.9.3.).

1.3.2. Sekundärliteratur

1 Rückseite des Buchumschlages

2 Rückseite des Buchumschlages

3 „*Patient, tolerant*“. Ahmed, Salahudin, 1999. A Dictionary of Muslim Names. London: Hurst and Company. S. 262

- Bertoncini-Zúbková, Elena. 1999. "Kenyan Literary Kiswahili", in: AAP. Köln: Institut für Afrikanistik der Universität Köln. 60, S. 45-58. (Z.1.26.60.).
- Björkman, Ingrid. 1989. "Mother, sing for me." People's Theatre in Kenya. London: ZED Books. (S.6.6.5.).
- Eastman, Carol M. 1981. "Kiswahili Diglossia in Kenya: Implications of Language Policy", in: Studies in African Languages. Suppl. 8, S. 20ff. (Z.1.12.).
- Eastman, Carol. "Waungwana na Wanawake: Ethnicity and Sex Roles in Islamic Coastal Kenya", in: Journal of Multilingual and Multicultural Development.
- Hanak, Irmi. 1996. „Language, Gender and Law: Divorce in the Context of Muslim Family Law in Zanzibar“, in: Journal of African Cultural Studies. London: SOAS. 9/1, S. 27-42. (Z.7.32.9/1.).
- Heine, Bernd/ Wiese, Bernd. 1969. Geographische Grundlagen der Verbreitung des Swahili in westlichen Kenya. Köln: Universität, Manuskript. 16pp. (B.8.15.1.).
- Mohochi, E.S. 2003. "Language Choice for Development: the Case of Swahili in Kenya", in: Journal of African Cultural Studies. London: SOAS. 16/1, S. 85-94. (Z.7.32.16/1.).
- Nelson, Nici. 1996. „Representations of Men and Women, City and Town, in Kenyan Novels of the 1970s and 1980s, in: Journal of African Cultural Studies. London: SOAS. 9/2, S. 145-168. (Z.7.32.9/2.).
- Obura, Oluoch. 1983. Die Entwicklung des Dramas in Kenya. Dissertation. München: Ludwig-Maximilians-Universität. (S.7.6.1.).
- Rhoades, Joan. 1977. Linguistic Diversity and Language Belief in Kenya: The Special Position of Swahili. Syracuse University. (B.8.15.9.).
- Rwezaura, Balthazar A. 1981. Sheria ya Ndoa Tanzania. Dar es Salaam: TUKI. 74pp. (B.8.13.61.).
- Salim, A.I. 1973. The Swahili Speaking Peoples of Kenya's Coast. Nairobi: EAPH.
- Schild, Ulla. 1980. "Words of Deception. Popular Literature in Kenya", in: Schild, Ulla (ed.). The East African Experience. Berlin: Reimer. S. 25-33. (S.6.6.1.).
- Wamitila, Kyallo Wadi. 1997. "Reading the Kenyan Swahili Prose. A Terra Incognita in Swahili Literature", in: AAP. Köln: Institut für Afrikanistik der Universität Köln. 51, Swahili Forum IV, S. 117-125. (Z.1.26.51.).

Siehe auch die Datei Swahili-Literaturliste auf dieser Website www.swahili-literatur.at

2. Texte
Matini

2.1. Personen
Wahusika

Abdalla	Geschäftsmann, ehemaliger Studienkollege Ahmads
Ahmad	Beamter im Informationsministerium Kenias
Ali	Vater Halimas
Amina	Eine Verwandte Halimas
Halima	Studentin an einer Pädagogischen Akademie in Nairobi. Freundin Ahmads
Hassan und Mjafa	Freunde Ahmads. Hassan ist Lehrer und Mjafa Chauffeur
Idi:	Onkel Halimas
Kijana (i.e. Junge)	Studienkollege Sofias
Mama Halima	Mutter Halimas
Mwendo:	Hausdiener Ahmads und Halimas
Rukia:	Freundin bzw. zweite Ehefrau Ahmads
Sofia:	Studentin an einer Pädagogischen Akademie in Nairobi. Freundin Halimas
Waziri:	Studienkollege Sofias

2.2. Theatertext
Tamthilia

2.2.1. Kitendo cha Kwanza. Onyesho la Kwanza.

Halima und Sofia befinden sich im Lagerraum der Sporthalle ihrer Akademie. Sie suchen den Spielball und das Netz, das sie dringend brauchen. Eigentlich hätte der Student Waziri, der für Sporthalle zuständig ist, diese Angelegenheit erledigen sollen, aber er ist noch nicht da.

Das Gesprächsthema ändert sich, als Halima Sophia einen Brief zeigt.

Sofia: (Macho yanamwangaza.) Ohoo; ndiyo ile barua ya Ahmad?

Halima: Isome haraka twende zetu, bwana⁴.

Sofia: Halima.

Halima: Labeka.

Sofia: Unampenda kweli Ahmad? Maana ikiwa humpendi hasa usimruhusu aharibu pesa zake zote hizi. Kwani hii itakuwa ni dhuluma.

Halima: (Kimya) Kwa kweli sijui hasa kama nampenda kama anipendavyo. Lakini natu...

Sofia: Basi siku zote yeye anaharibu pesa na wakati wake. Anakununulia mavazi adimu adimu; anakuja kukutembelea amebeba zawadi tunu tunu.

Halima: Labda nitampenda katika siku zijazo kwani kila jambo lina mwanzo. Lakini naona umesahau kuwa huu ni wakati wa michezo.

Sofia: Sikusahau kamwe. Angalia, kama tukizungumza kwa dakika tano zaidi tutachelewa tu mchezoni. Hakuna atakayepata hasara.

4 Gemeint ist Sophia

Halima: (Anacheka.) Nhu.

Sofia: Lakini tusipochungua kama unampenda Ahmad ujue atafanya gharama kuja huku kukuona. Nayo ni hasara kwake.

Halima: Basi wewe nipe wasaa nami nitajaribu kuushawishi moyo wangu.

Sofia: (Anavuta hatua.) Mhurumie Ahmad. Amekutendea kiungwana tangu siku mliyoanza urafiki na ikiwa kweli nawe u mwungwana utakumbuka kuwa “mtenda mema hulipwa mema⁵”.

Halima: (Anamfuata huku anacheka.) Acha kunihubiria, Sofia. Wewe wajifanya walii sana na ni juzi tu ulipompiga Juma kalamu bila ya makosa yoyote! (*Kimya*).

Sofia: Nitakwambia neno moja, Halima.

Halima: Ehe.

Sofia: Huyu alikuwa kijana asiyejua ustaarabu ni kitu gani. Nami nilimtendea kama alivyostahili. Lakini Ahmad hatastahili kutendewa hivyo.

Halima: Unanichokesha na maneno haya.

Sofia: Afadhali ukate shauri sasa ama utamvunja moyo Ahmad atakapobaini baadaye kuwa wakati wote huu ulikuwa unamhadaa.

Halima: Haya basi nimekubali. Nitajishauri.

Sofia: Pole Halima. (*Anatabasamu.*) Sina shaka nimekutia matatani kwa kukucheleweshwa namna hii. (*Uk. 2-3*).

Zwei Studenten stützen Waziri, der beim Fußballspiel verletzt worden ist. Halima kümmert sich sehr um Waziri. Sie holt Medikamente und verbindet seine Wunde mit ihrem eigenen Kopftuch. Auch Sofia hilft mit. Halima und Sofia gehen ins Studentenheim, nehmen ein Bad und gehen danach in die Mensa zum Abendessen.

2.2.2. Kitendo cha Pili. Onyesho la Kwanza.

Halima, Sofia, Ahmad sowie seine Freunde Hassan und Mjafa sitzen in der Wohnstube Ahmads. Der Gastgeber ist vornehm gekleidet. Da Halima und Sofia sich auf das Lehramt vorbereiten, dreht sich das Gespräch naturgemäß um die Schule. Hassan ist Lehrer schon seit fünf Jahren.

Hasan: (Anatabasamu.) Tutakapokutana tena labda sitakuwa mwalimu.

Halima: Kwa nini?

Hassan: Nataka badilisha (kubadilisha) upepo. Nimekuwa mwalimu kwa miaka mitano sasa. Na jinsi wanavyozidi wenzangu kwenda mbele, ndiyo mimi hurudi nyuma.

Sofia: Unatuvunja moyo basi.

Hassan: La, sivyo. Wewe angalia hali ya mwalimu. Anawasomesha watoto wakiwa darasa la saba. Miaka saba baadaye wanakuwa watu wa vyeo. Na kila upitapo mwaka, umbali kati ya mwalimu na mwanafunzi wake wa zamani unazidi.

Sofia: Lakini sio wote wanaopata vyeo hivyo?

Hassan: Nakubali sana. Lakini wale wachache wapatao ni katika jumla ya wanafunzi wake. (*Kimya*)

Mjafa: Sioni kwa nini useme hivi. Kwani wewe unajua tangu kitambo na kabla hujaanza kazi kuwa ualimu ni kazi ya kujitolea kusaidia ulimwengu. Ni kazi ya „Harambee”⁶. (*Wanatabasamu.*)

Wote: Naam, naam. Unasema kweli.

5 Redewendung

6 In den 70er Jahren des vergangenen Jahrhunderts war es üblich die nationale Pflichtideologie in der Literatur zu erwähnen.

Hassan: Kabla sijajiuzulu katika ubishi huu nataka kusema kitu kimoja.

Ahmad: Hebu sema tusikie.

Hassan: Mimi sikubali na neno “harambee“ tunapozungumza habari hii ya ualimu na pia habari nyingenezo.

Ahmad: Utakataaje bila sababu ?

Hassan: Sababu yangu ni moja tu: kuwa katika kuvuta harambee hii kuna wale wavutao kamba hasa. Na kuna wale walioketi chini kushangalia kamba ikivutwa. Na sote wanaovuta na wasiovuta twaambiwa twavuta “harambee”.

Sofia: Fafanua fumbo hili, bwana.

Hassan: Wako wanaobania mijishahara mikubwa mikubwa. Kwa sababu Serikali haina pesa, wanaombwa watoe idhini mijishahara hiyo ikatwe ndiyo walimu wapate nyongeza. Lakini wapi? Walimu tutabaki papo hapo tukung’ang’ania kamba kavu.

Sofia: Nimetayarisha chai huko chumbani kwa wageni. Mimi nitakwenda na Mjafa na Hassan halafu nyinyi mtanifuata baadaye.

Ahmad: Asante, Sofia, kwa kutukirimu. (*Uk. 6-7*).

Der eigentliche Grund des Besuchs ist eine Gelegenheit für Halima und Ahmad, einander näher kennen zu lernen. Sie sind jetzt allein.

Ahmad: (...) Je, habari za masomo?

Halima: Njema. Je, za kazi?

Ahmad: (*Anamgeukia.*) Vivyo hivyo.

Halima: Je, kuna mzozo wo wote?

Ahmad: Huwezi hasa kuuita mzozo kwani si mzozo. Lakini wale jamaa wakubwa kule nasikia fununu kuwa wanataka nibadilishwe.

Halima: Kwa makosa gani? Au waona kuwa waweza ukapata nguvu nyingi hapo ulipo?

Ahmad: He, Halima! Macho yako yanaona mbali siku zote. Lakini sivyo; wajua kule katika Jimbo la Kaskazini hakuna ofisi kubwa ya Wizara ya Habari. Basi sasa wanataka kuanzisha moja huko.

Halima: Na kwa nini wakupeleke wewe? Nina hakika kuna watu wengine wawezao kwenda huko.

Ahmad: Ndiyo; lakini wanadai kuwa mimi kazi hii nimeifanya siku nyingi na kuwa nikipelekwa huko nitahakikisha kuwa makosa katika siku za kwanza yatakuwa machache.

Halima: Ni hivyo, eh?

Ahmad: Ni hivyo. Lakini Halima ...

Halima: Labeka⁷.

Ahmad: Mbona una wasiwasi juu ya kubadilishwa kwangu?

Halima: Nina wasiwasi maana naona wewe mwenyewe huna wasiwasi.

Ahmad: Vipi?

Halima: Basi ukiwa huna wasiwasi nawe wajua ukienda huko kuonana kwetu kutakuwa kwa shida, nitakosaje kuwa na wasiwasi? Labda umeshabadili nia, je? Ndiyo sababu ukatokwa na wasiwasi ?

Ahmad: La, si hivyo, Halima. Kwa nini? Nikibadilishwa, nitabadili maskani tu bali ile nia na mapenzi yatabaki nawe daima.

Halima: Nhu.

Ahmad: Na Halima ...

⁷ Wenn eine Frau beim Namen angerufen wird, antwortet sie „Labeka“ oder „Be“, der Mann antwortet „Naam“.

Halima: Labeka.

Ahmad: Nimeingiwa na wasiwasi, mpenzi, juu yako.

Halima: (Anagutuka.) Wa nini?

Ahmad: (Anasita.) Sasa wewe u karibu kuhitimu masomo yako. Na kama ujuavyo ukishahitimu posa nyingi utapokea.

Halima: Unaniudhi sasa. (Uk. 8-9).

Bevor sie sich wieder zu den anderen gesellen, erinnert Halima Ahmad an etwas:

Halima: „Ndiyo, lakini hujanieleza habari ya lile shamba ulilotaka kununua huko nyumbani.“ (Uk. 10).

2.2.3. Kitendo cha Pili. Onyesho la Kwanza.

Um die Mittagszeit im Hause Ahmads in Changamwe. Das Wohnzimmer ist schön und luxuriös ausgestattet. Es gibt viele Bücher in den Regalen und auf dem Tisch. An den Wänden hängen schöne Gemälde. Halima, die Ahmad inzwischen geheiratet hat, kommt herein. Sie trägt ein teitei (elegantes Abendkleid) und raucht eine Zigarette. Sie schaltet das Radio ein, schaltet es aus, öffnet ein Buch, liest ein wenig darin und schließt es wieder. Sie schaut zu den Bildern an der Wand. Sie löscht die Zigarette und zerdrückt sie. Sie langweilt sich. Sie ruft den Hausdiener Mwendo.

Halima: Mwendo (Kimya) (Anainua sauti.) Mwendo.

Mwendo: (Anajibu akiwa ndani.) Naam.

Halima: Hebu.

(Mwendo - kijana mfupi na mnene mwenye uso mpana anaingia amebeba kijisufuria mkononi na sabuni mkono mwingine.)

Mwendo: Naam?

Halima: (Anavuta kiti na kuketi chini. Anapapasa mfuko wa teitei; anatoa sigara na kiberiti.) Unafanya nini jikoni?

Mwendo: Naosha vyombo.

Halima: (Anatoa kijiti cha kiberiti.) Tangu ulipopika chai mpaka sasa waosha vyombo?

Mwendo: Baada ya kuwaandalia kiamsha-kinywa, nilikwenda sokoni kutafuta mboga.

Halima: Kwani wataka kupika nini?

Mwendo: Chenga.

Halima: (Anakunja uso.) Hizi chenga haziwachokeshi? Kila siku chenga mpaka lini?

Mwendo: Ndizo Ahmad apendazo.

Halima: Tangu leo itakubidi ubadilishe mapishi. Mimi sikuzoea kulishwa chakula kimoo-ja tu kama farasi. (Uk. 11-12).

Sofia kommt herein.

Halima: (Anatabasamu.) Ni wewe Sofia?

Sofia: (Anampa mkon.) Ni mimi, Halima.

Halima: Haya karibu, basi. Keti chini.

(Wanaketi. Wameelekeana.)

Sofia: Habari za huku?

Halima: (Kwa sauti dhaiifu.) Njema tu. Na wewe ulikuja lini?

Sofia: Nilikuja jana.

Halima: Kwani chuo cha walimu kimeshafunguliwa?

Sofia: Tutafungua leo.

Halima: (Anawasha sigara.) Alaa.

(Mwendo anatoka.)

Sofia: Ndiyo kwanza uamke au vipi?

Halima: Nifanye nini dada yangu isipokuwa nilale mpaka sijui saa ngapi?

Sofia: (Anatabasamu.) Una starehe basi.

Halima: Starehe gani, dada?

Sofia: Jumba hili lote ni lako! Bwana'ko Ahmad ndiye msaidizi wa Mkuu wa Idara ya Habari katika Jimbo la Pwani! Isitoshe basi: utakacho hukosi maana mapesa kwake si kitu.

Halima: (Anashika tamaa.) Wewe tu ndiye uwezaye kusema hivyo.

Sofia: Kwa nini?

Halima: Laiti ungejua dhiki nipatayo hapa, hilo hungelitamka.

Sofia: Dhiki gani upatayo? Chakula kiko ghalani; vifaa viko makabatini; akiba iko benki.

Halima: (Kwa sauti ya kutweza.) Maisha si kula na kunywa tu; kuna...

Sofia: Kuna nini zaidi ya hayo?

Halima: Kuna starehe pia.

Sofia: Ungeomba starehe gani baada ya hii upatayo hapa na kila kitu unacho?

Halima: Wasema hivyo maana humjui Ahmad! Hatwendi (Hatuendi) sinema; hatwendi kupunga upepo baharini; hatwendi matembezi; ajualo yeye ni kula na kulala tu.

Sofia: Nawe kuolewa si juzi juzi tu? Si bado anangoja utue kwanza.

Halima: Aaa! Maisha haya ya kufungwa ndani kwa ndani siyawezi miye.

Sofia: (Anakaza sauti.) Kumbuka kuwa umeshaolewa sasa si pale ulipokuwa huru kama msichana.

Halima: Ndiyo; lakini maisha hayaendi hivi ati. Lazima kuwe na mabadiliko hapa na pale: leo tukila sembe kesho tule wali; leo tukienda sinema kesho tushinde nyumbani. Lakini ati maisha vuguvugu kama bahari hayawezekani. (*Sofia ameduwaa huku anamwalia tu.*) Hata hiyo bahari hubadilisha umbile: mara ichafuke, mara iwe shwari; mara maji yajae, mara yakupwe.

Sofia: (Anacheka ndani kwa ndani.) Nilidhani fikira hizi utaziacha ukiolewa. Sasa nakuona unazo vile vile. Nasi tutafanya nini?

Halima: Kwa nini?

Sofia: Ikiwa maisha ya kuolewa ni kama hayo usemavyo.

Halima: Siwezi kukushauri uolewe, dada. Lakini hayo tuyaaache. Je, sasa umebakiza siku ngapi umalize?

Sofia: Miezi miwili hivi halafu nitafanya mtihani.

Halima: Halafu utakuwa mwalimu wa cheti.

Sofia: Natumaini hivyo.

Halima: Mungu atakujalia. (Uk. 12-14).

Ahmad tritt ein. Er trägt einen schwarzen Anzug und ein weißes Hemd. In der Hand hält er eine Zeitung. Nach kurzer Begrüßung und Gespräch mit Sofia teilt er Halima mit, daß er eine Dienstreise vor sich habe. Sofia verabschiedet sich, denn sie möchte rasch zur Pädagogischen Akademie zurückkehren. Kaum haben Halima und Ahmad angefangen miteinander zu sprechen, geht schon der übliche Streit los.

Halima: Utakwenda lini huko wendako?

Ahmad: (Anaendelea na kusoma.) Kesho asubuhi. Nilifikiri baba ataleta barua leo lakini nimeangalia sikuona kitu.

Halima: Nawe tangu uandike barua ni lini?
Ahmad: Juma moja hivi. (*Mwendo anamletea chai halafu anatoka.*)
Halima: Ya nini?
Ahmad: Nilikuwa nataka kujua kama alipata fedha nilizomtumia anunue mbolea ya shamba.
Halima: Zile shilingi mia moja zote ulimpelekea?
Ahmad: Ndizo nilizokuwa nikitaka kujua kama amezipata.
Halima: (*Anachukua gazeti.*) Na wewe na shamba hili!
Ahmad: Lina nini?
Halima: Kila mwezi ni lazima upeleke shilingi mia moja, kila mwezi!
Ahmad: Na kama haliangaliwi watu watakula nini?
Halima: Basi si kila mwezi.
Ahmad: Ndiyo. Lakini kila mwezi sipeleki pesa huko; kuna skuli yataka kujengwa huko. Nami natoa sehemu yangu ya mchango.
Halima: Sioni kwa nini ujishughulishe na mambo ya huko. Kwa nini huwaachii wenyewe?
Ahmad: Hata mimi ni mwenyewe.
Halima: U wenyewe vipi? Huna mtoto anayesomea huko. Na nduguyo pia hajaingia skuli.
Ahmad: Ndiyo; lakini huko ndiko kwetu nami imenipasa nisaidie katika maendeleo yanayofikiriwa. (*Anasimama aingie ndani.*)
Halima: Tuseme basi hatujajifurahisha kwa njia yoyote?
Ahmad: (*Anazunguka kumwangelia.*) Ati nini?
Halima: Ulisema tutakwenda Malindi, mpaka leo hatujaenda.
Ahmad: Wakati nilikuwa sina senti pia nilikujulisha kuwa zilikuwa haba. Watakaje sasa. Zikipatikana mwisho wa mwezi tutakwenda. (*Anaangalia ndani.*) Oh pole. Kweli. Tumeshaaifikiana na mwenyewe juu ya bei na kila kitu. Na hati ya shamba hilo atanitumia karibuni.
Halima: Na ni nani atakayeliangalia nawe uko huku?
Ahmad: Hilo sijajua bado. Lakini nitakapopata hati yenyewe nitakamilisha mipango yote.
Halima: Basi huna wasiwasi sasa.
Ahmad: (*Anajikuna kichwa.*) Wasiwasi bado uko; kwani ndio kanzu yetu. Na twende mashariki au magharibi wasiwasi tunao tu.
Halima: (*Anagutuka.*) Wa nini tena nami nilidhani shamba ndilo lililokutia mashaka?
Ahmad: Ni habari ya ile shule (vorher: skuli) ya watoto kule nyumbani.
Halima: Waitakia nini shule hiyo nawe u mbali na huko?
Ahmad: (*Anasimama na kuzungukazunguka sebuleni.*) Nilipokea barua ya kamati ya shule hiyo. Nayo yaniomba niwe nikitoa sehemu yangu ya mchango kusaidia uendeshaji wake.
Halima: Watakia nini mambo hayo? Kumbuka kuwa asiyekuwako na lake haliko⁸.
Ahmad: Nitakueleza baadaye ila sasa tutoke tukawatafute akina Hassan waliko.
Halima: Haya basi twende lakini mambo haya (*Wanatoka.*) (*Halima huku ameshika tamaa.*) Aaa. Maisha haya hayawezekeani. (*Uk. 15-16.*)

Halima ist frustriert.

8 Sprichwort: *Asiyekuwapo (asiyekuwepo), na lake halipo.* (Syllables 6+6). *He who is not there, his share is not there, too.* Intentional meaning: *He who is not present will be ignored. If you want to benefit from an undertaking, take an active part in it.*

2.2.4. Kitendo cha Pili. Onyesho la Pili.

Zwei Tage später hat Halima Besuch von ihrer Verwandten Amina. Beide sitzen gemütlich in der Wohnstube. Amina trinkt Tee und Halima liest ein Buch. Zwischendurch plaudern sie. Das Gespräch kreist um Ahmad. Amina ist nämlich gekommen, um eine Scheidung von Ahmad und die beabsichtigte neue Ehe mit Abdalla zu besprechen.

Amina: Hayo basi ndiyo niliyokuwa naja kukueleza. Mwenyewe utajua la kufanya.

Halima: Hata mimi aliniletea barua.

Amina: Nani, Abdalla?

Halima: Ehe.

Amina: Ndiyo; lakini sasa anataka habari ya ndoa.

Halima: Ninyi ndiyo (ndio) mlioleta mzozi huu wote.

Amina: Vipi tena?

Halima: Pale kwanza, Ahmad alipokuja kuniposa mimi nilimkataa, nikasema namtaka Abdalla. Mkakataa. Leo imekuwaje tena mnamkubali?

Amina: Tulikuwa tukiona kuwa Ahmad ana kazi ya madaraka makubwa na hivyo ataweza kukupatia maisha mazuri. (...).

Halima: Nimeshakwambia (nimeshaambia *oder* nimekwisha kukuambia) Ahmad kuwa maisha haya hayavumiliki. (*Uk. 17*).

Ahmad ist zwar in der vorigen Nacht spät von seiner Dienstreise zurückgekehrt, muß aber schon früh ins Büro gehen, um seine Versetzung nach Isiolo vorzubereiten. Halima möchte zunächst nicht dorthin übersiedeln, denn die Gegend ist heiß und es gibt wenige gute Geschäfte dort. Ahmad möchte sie auch nicht sofort mitnehmen, denn er will die Zustände dort zuerst erkunden.

Ahmad: (*Anatabasamu.*) Shikamoo, mama.

Amina: Marahaba, mwanangu. Je, habari za siku nyingi?

Ahmad: (*Anaketi.*) Njema. Sijui za huko nyumbani.

Amina: Njema.

Ahmad: Halima alinieleza kama ulikuja mchana nilipotoka safari usiku.

Amina: Amenieleza kuwa ulirudi usiku.

Ahmad: Je, wakwe zangu wambaje?

Amina: Hawajambo. (*Halima anatoka.*)

Ahmad: Je, habari zaidi?

Amina: Nilikuwa nimekuja kwa sababu ya Halima.

Ahmad: Ana nini Halima?

Amina: Nduguye aliyezaliwa hivi majuzi atatoka nje kesho kutwa.

Ahmad: Ehe.

Amina: Ndiyo nilikuwa nataka umpe ruhusa twende naye.

Ahmad: Kwa nini?

Amina: Ili awe huko nduguye akitoka arobaini.

Ahmad: Je, asipohudhuria itakuwaje?

Amina: Atakuwa amevunja mwiko.

Ahmad: Mambo haya ya kizamani sasa yamezikwa, Mama. Ikiwa nduguye hataridhika, kuna ubaya gani asipohudhuria?

Amina: Ndiyo, lakini ni mila.

Ahmad: (*Anasimama.*) Mila ngapi, Mama, hazifuatwi siku hizi? (*Uk. 18-19*).

Ahmad will, daß Amina in der Wohnung bleibt, während er dienstlich in Isolo ist. Amina ist enttäuscht.

2.2.5. Kitendo cha Pili. Onyesho la Tatu.

Vier Tage nach dem Besuch Aminos kommt Ahmad müde von der Reise nach Hause. Er findet die Wohnstube in einem unordentlichen Zustand. Sofia klopft an und kommt herein. Sie möchte Halima besuchen.

Ahmad: (Anampa mkono.) Je, Sofia, habari gani?

Sofia: Njema.

Ahmad: (Anainua kiti kilichoanguka sakafuni.) Keti basi.

Sofia: (Anaketi) Je, kuna nini mbona kila kitu kimeondolewa mahali pake?

Ahmad: (Naye pia anavuta kiti cha kuketi.) Hata nami nauliza hivyo.

Sofia: Na Halima naye amekwenda wapi?

Ahmad: Usiniulize, bwana.

Sofia: Kwa nini?

Ahmad: Kwa kuwa sina nijualo kuhusu mahali alipo. Kwani naambiwa kuwa ametoka na mkasa mjombaye. (Mwendo anarudi ndani.)

Sofia: Alikuwa lini mkasa mjombaye?

Ahmad: Ana kama siku nne hivi.

Sofia: Labda watarudi hivi punde basi.

Ahmad: Hilo sijui mimi. Ni vigumu sana wao kurudi.

Sofia: Kwa nini?

Ahmad: Mwendo aliniambia kuwa Halima alikuwa amechukua sanduku. Na mkaza mjombaye amebeba furushi.

Sofia: (Anajaribu kuficha mshangao.) Nilikuwa naja kumjulisha Halima kuwa kuna msichana mmoja tunayesoma naye atakayekwenda nyumbani kesho; kama mna ujumbe atawafikishia nyumbani.

Ahmad: Yeye mwenyewe ashajipelekea basi.

Sofia: Unafikiri amekwenda nyumbani?

Ahmad: Nitakosaje kufikiri hivyo.

Sofia: Ikiwa hakukuwa na maneno kati yenu, basi hawezi kwenda kwao.

Ahmad: Maneno hatukuwa nayo.

Sofia: Basi utajua leo leo alikokwenda na kilichomfanya aende.

Ahmad: Labda.

Sofia: (Anasimama.) Nami nataka kutoka sasa.

Ahmad: Mara moja hii?

Sofia: Nataka kupitia madukani kabla sijarudi chuoni.

Ahmad: (Anasimama.) Twende basi nikusindikize. (Wanatoka.). (Uk. 22-23).

Ahmad begleitet Sofia zur Haustüre. Sie verabschieden sich.

2.2.6. Kitendo cha Tatu. Onyesho la Kwanza.

Es ist Abend. Amina und Halima befinden sich in Alis Haus, in der Stadt Kibwezi. Die Wohnung sieht ärmlich aus, die Wände sind vom Rauch geschwärzt, die Bettwäsche zerrissen, auf dem Lehm Boden liegen Fetzen und die Möbelstücke sind mit Staub bedeckt. Da es an Stühlen mangelt, sitzen Amina und Halima auf dem Bett, Abdalla auf

dem einzigen vorhandenen Stuhl.

Abdalla steht im mittleren Alter, etwa zwischen 30 und 40. Er hat einen Laden in Kibwezi und einen in Mombasa. Den Laden in Kibwezi möchte er verkaufen und das Geld in ein Holzwarengeschäft investieren. Während er noch mit ihnen plaudert, kratzt er sich die Beine, wo sich einige Flöhe eingensistet haben. Abdalla und Amina tauschen ihre Gedanken über Frauen und Ehe aus.

Abdallah: (Anajikuna miguu ambayo imesha nyemelewa na viboroto.) Inshallah. Je, Sofia hajarudi bado?

Halima: Nilikuwa naye kabla sijaja na alinieleza kuwa atamaliza masomo yake mwakani.

Abdalla: Afadhali asome maana imekuwa mtu hana akiba siku hizi ila masomo.

Amina: (Anamkinga Halima.) Ah! Lakini nao hao wasichana wanaosoma hawaoleki tena.

Abdalla: Kwa nini?

Amina: Ikishakuwa utaoa mke, halafu awe hana nafasi ya kukutumikia tena. Akiondoka asubuhi ale kiamshakinywa aende zake kazini; saa saba aje ale arudi kazini! Hatapata nafasi ya kukupikia wala kukufulia nguo!

Abdalla: Mume na mke wakiwa na busara hiyo si shida ambayo haiwezi kukubaliwa. Tena hali ya maisha haiwezekani mpaka mume na mke wafanye kazi wasaidiane gharama za watoto na za nyumbani.

Amina: (Anamwangalia Halima aliyeinamia chini.) Najua hivyo ndivyo wasemavyo vijana wanaofanya kazi, lakini wote watakujakubali kuwa mke ni yule amtumikiaye bwanaye.

Abdalla: Lakini ikiwa mume hana nguvu za kumlisha mkewe, mkewe atamtumikia vipi? Na ikiwa ni lazima wasaidiane gharama, basi mke amsaidie mumewe hata ikiwa itambidi aingie kazini.

Amina: (Anajikuna miguu.) Mke afanye kazi? Hilo halikusikilikana zamu zetu tulipokuwa wasichana"

Abdalla: Na maisha nayo hayakuwa yenye gharama kubwa hivi yalivyo sasa.

Amina: Ni kweli.

Abdalla: Hivyo basi naona ni heri watoto wetu tuwaelimishe wote wavulana kwa wasichana. Msichana asipoolewa au akipewa talaka ataweza kujitafutia riziki bila ya kujitia aibu. (Uk. 25).

Amina, die von dieser Argumentation nicht ganz überzeugt ist, meint, daß auch Frauen, die nicht studiert haben, heiraten können und glücklich sind. Abdalla antwortet:

Abdalla: Kila mtu tonge lake⁹. (Uk. 26).

Mzee Ali, ein kleiner dicker Mann kommt herein. Er trägt ein kanzu ya hudhurungi und ein kofia nyeupe ya mkono, die Kleidung der (Waswahili) Küstenbewohner. Da er arbeitslos ist, bietet ihm Abdalla eine Stelle als Aufseher in seinem Holzgeschäft an, falls das Unternehmen gelingt.

2.2.7. Kitendo cha Tatu. Onyesho la Pili.

Es ist Nacht. Halima und Abdalla befinden sich im gleichen Zimmer, wie in der vorigen

9 Redewendung

Szene. Halima sitzt auf dem Bett und Abdalla auf dem Stuhl.

Halima erzählt Abdalla von den Problemen, die sie mit Ahmad gehabt hatte. Abdalla kennt ihn gut. Sie waren Schulkameraden. Ahmad war immer ein Arbeitstier und hatte wenig Verständnis für Frauen, Liebe und Freizeit.

Abdalla: (...) Mwulize habari za mashamba na kujenga mahospitali tu. Hana jingine.

Halima: Basi mtu si hutamani kwenda dukani. Yeye alikuwa fundi wa kununua vifaa na viungo vyote vikae ghalani. Husemi ni ng'ombe wanaolishwa.

Abdalla: Basi vitu kama unga si utaota uyoga au viazi vioze?

Halima: Kwake si kitu.

Abdalla: Basi ni nani atakayeweza maisha kama hayo?

Halima: Anadhani watu wote ni kama yeye.

Abdalla: (Anaondoka na kwenda kuketi juu ya kitanda kuliani pa Halima.) Anajua nini kuhusu mapenzi au maisha ya mke na mume?

Halima: Atajua mwenyewe.

Abdalla: (Anamshika Halima mkono wa kulia.) Hajui kwamba mke ni chombo na nahoda asipoushika usukani vizuri chombo kitakwenda mrama?

Halima: (Anajitingisha huku anatabasamu.) Hebu hayo tuyaaache; jina lake nikisikia moyo unaniruka kama kwamba nimeletwa ilani ya kuwa malaika wa kifo yuko njiani ananijia.

Abdalla: Sasa nataka kujua Halima, (Anamsogelea.) kama wanipenda au ni yale maneno watoto wanayonong'onezana.

Halima: Kama nilikuwa sikupendi, (Anamwangelia.) nisingehatarisha hayo niliyohatarisha.

Abdalla: Yote hayo ni maneno tu. Sasa nataka tuyatimize kwa kufunga ndoa.

Halima: Mimi ni tayari. Lakini itatupasa tumsubiri Ahmad.

Abdalla: Ahmad ana kazi gani tena?

Halima: (Anacheka.) Hukumbuki kuwa mimi ni mkewe kwa sheria bado?

Abdalla: Ndiyo lakini lazima akuache.

Halima: Natumai hivyo. Kwani asiponiacha yeye mimi siwezi kuolewa.

Abdalla: Akidinda tutazinunua talaka kutoka kwake.

Halima: Labda hivyo.

Abdalla: Hata ya nini kuzinunua? Mimi nitakufanyia mpango wende (uende) katika Chuo cha Walimu kwa muda wa miaka miwili.

Halima: (Anakunja uso.) Nhu.

Abdalla: Hata utakapomaliza na kupata shahada ya ualimu, atakuwa ameshakata tamaa ya kukupata tena, naye atakupa talaka tu.

Halima: Tutajaribu.

Abdalla: Waeleze Baba na Mama mpango huo. Halafu unipe jawabu, au wasemaje?

Halima: Haya.

Abdalla: Sasa acha niende. (Anasimama.) Na ukipata nafasi tutakwenda sinema kesho jioni. (Uk. 27-29).

Idi kommt herein, als Abdalla gerade weggeht.

Abdalla: Je, Bwana Idi hujambo?

Idi: Sijambo.

Abdalla: Na mimi natoka. (Anatoka haraka haraka.)

Idi: Ni nani huyo?

Halima: Ni Abdalla.

Idi: (*Anajaribu kwa nguvu kujikaza.*) Alikuwa amekuja tafuta (kutafuta) nini?

Halima: Alikuwa kaja kutuamkia.

Idi: Mbona tangu siku hizo simwoni? Au nyumba imeingia watu ulipotoka Mombasa?

Halima: Hata pia ameahidi kumpatia Baba kazi.

Idi: (*Anavuta kiti na kukaa.*) Habari hiyo sijui. Kama hili ndilo lililokulete naona utakuwa mzigo kwetu.

Halima: Basi hufai kusema hivyo kwani sikuja bure tu; na sababu zilizonifanya nije nimekwisha waeleza (kuwaeleza) nyote.

Idi: Hilo ni domo kaya tu. Kwani hakuna sababu iwezayo kumtoa mke kwa mumewe isipokuwa mume amehiari kumpa mkewe talaka. Leo wewe umekuja tu; hukutukanwa, hukupigwa, hukufukuzwa! Si domo kaya n'nini?

Halima: Afadhali mnifungie ndani basi niache kuleta balaa.

Idi: Hata ukifungiwa sandukuni, haifai kitu maadam umeshakuja nyumbani.

Halima: Na sasa nifanye nini?

Idi: (*Anasimama.*) Hilo utamwuliza msiri wako. Nijualo mimi ni kuwa umejitwika mzigo ambao maisha yako hutajibandua. (*Anatoka.*). (*Uk. 29-30*).

2.2.8. Kitendo cha Tatu. Onyesho la Tatu.

Eines Abends, etwa eine Woche später, befinden sich Mzee Ali, Mama Halima, Amina, Ahmad und Mwendo im gleichen Zimmer wie in der vorigen Szene. Es ist jetzt sauber und aufgeräumt und einige Stühle aus dem Nachbarhaus stehen drinnen. Es geht um Versöhnung zwischen Ahmad und Halima. Halima selbst aber ist nicht anwesend. Amina beginnt mit einer negativen Bewertung der Lage.

Amina: (...) yaonekana kuwa mambo yameharibika shinani; na mti ni lazima uanguke ikiwa shina limekwisha haribika. (*Uk. 31*).

Danach spricht sie von den Fehlern, die Ahmad begangen hat: Er hat ihr keine Erlaubnis gegeben, eine Familienfeier zu besuchen und er hat ihr nicht gestattet, allein einkaufen zu gehen. Ahmad verteidigt sich. Er hätte ihr nicht verboten, an der Familienfeier teilzunehmen, sondern nur um Zeit zum Überlegen gebeten. Sie ist aber ohne sein Wissen und ohne seine Zustimmung zu ihren Eltern zurückgekehrt. Er wollte sie nicht allein einkaufen gehen lassen, der Umgebung wegen.

Nachdem Amina ihre Ansichten geäußert hat, bittet Ahmad Mzee Ali, doch das Schlußwort zu sprechen und seine Meinung zu äußern. Mzee Ali bittet noch um einen Tag Bedenkzeit. Ahmad äußert den Wunsch mit Halima sprechen zu dürfen. Er wird ihm gewährt. Die Eltern Halimas, Amina und schließlich Mwendo verlassen das Zimmer. Halima aber zeigt wenig Interesse an einem versöhnenden Gespräch. Sie weigert sich das Zimmer zu betreten und bleibt an der Türschwelle stehen.

Ahmad: Je, Halima, u hali gani?

Halima: Njema. (*Mwendo anatoka.*)

Ahmad: Pita ndani. Mbona umesimama kizingitini?

Halima: Panatosha hapa.

Ahmad: Nimekuja kujua kisa kilichokutoa nyumbani.

Halima: Hukutosheka na visa niliyokusimulia tulipokuwa sote Mombasa?

Ahmad: Hivyo vilivyo visa vya kinyumbani, na tuliishi pamoja tukiwa na visa hivyo.

Lakini hiki cha leo ni tofauti kwani ndicho sababu ya kuja kwako kwenu.

Halima: (Anainuka.) Utanisamehe maana nina chungu jikoni na huo wakati wa kuvikariri sitaupata.

Ahmad: Halima, wewe ni mtu wa kuniambia mimi huna wakati?

Halima: Kwa nini?

Ahmad: Hukumbuki hisani yangu?

Halima: Nikishakumbuka ndio nifanye nini?

Ahmad: Basi kama huna la kufanya jua hivi ...

Halima: Vipi?

Ahmad: Kuwa hata mimi sina wasaa wa kukariri wema tuliotendeanana tulipokuwa pamoja. (...). (Uk. 33).

Ahmad erkennt nun, daß ein weiteres Gespräch keinen Sinn hat. Er verabschiedet sich höflich von seiner Gattin, was sie an der Türschwelle schweigend zur Kenntnis nimmt.

2.2.9. Kitendo cha Tatu. Onyesho la Nne.

Eines Nachmittags im Hause Mzee Alis. Amina und Halima sitzen in der Wohnstube und erörtern die Möglichkeit einer Ehescheidung. Halima fürchtet jedoch, daß Ahmad die Scheidung ablehnen werde, denn er steht im Vorteil.

Halima: Je, akikataa?

Amina: Akikataa ana nini? Tutazinunua.

Halima: Mume huuza talaka akiwa na haja ya kulipa gharama alizozimfanyia mkewe.

Amina: Hata Ahmad anataka kujilipa tu. Kwani kama ni mwungwana hangengoja tumtajie pesa, ndio akupe talaka. Angekuacha tu kukuonyesha kuwa wewe siye msichana pekee.

Halima: Lakini Ahmad hataki kujilipa tu. Ana mengi moyoni mwake.

Amina: Moja kama lipi?

Halima: Yeye anajua kuwa anaweza kuoa wakati wowote, lakini mimi siwezi kuolewa kabla yeye hajaniacha. Naye aweza kuzizuia talaka hizo kama sehemu ya adhabu atakayonipa; naye ana hakika kuwa akifanya hivyo atayakamua matumaini kutoka katika maisha yangu.

Amina: Umeshasahau kuwa kuna kadhi?

Halima: Nawe umeshasahau kuwa kadhi hawezi kumlazimisha anipe talaka ikiwa makosa ni yangu? (Uk. 35-36).

Halima weiß, daß es nicht möglich sein wird, die Scheidung gerichtlich vor einem khadi zu regeln, denn es läuft das Gerücht um, daß Halima Abdalla heiraten möchte, weil dieser reicher als Ahmad ist. Es hat sich auch herumgesprochen, daß Mzee Ali in der Holzwarenhandlung Abdallas eine Stelle bekommen soll, als Gegenleistung für seine Vermittlung der Ehe mit Halima.

Amina versucht herauszufinden, warum Abdalla dieser Tage Halima so selten besucht. Sie vermutet, daß Abdalla die Hoffnung auf eine Scheidung zwischen Halima und Ahmad aufgegeben hat. Abdalla weiß, daß Ahmad nicht leicht nachgeben wird. Inzwischen hat Abdalla auch zu erkennen gegeben, daß er eher einen Aufseher mit Schulausbildung, der sich auch im Fachbereich Holz gut auskennt, anstellen wird.

Sie wechseln das Thema, gehen in die Küche und bereiten sich ein Essen zu, denn beide

haben Hunger.

2.2.10. Kitendo cha Nne. Onyesho la Kwanza.

Etwa zwei Monate später. Ahmad sitzt in seiner Wohnstube in Changamwe, Mombasa. Auf dem Tisch liegen viele Bücher. Er lebt mit einer jungen Frau namens Rukia zusammen.

Ahmad: (Anafunga kitabu.) Rukia.

Rukia: (Anajibu akiwa ndani.) Labeka.

Ahmad: Hebu njoo.

Rukia: (Anampa chai na kuketi kando yake.) Basi nawe Ahmad hupumziki?

Ahmad: (Anamwangukia kwa mapenzi.) Kwa nini?

Rukia: Tangu asubuhi uko kazini, ukija nyumbani aidha utaandika barua au uanze kusoma!

Ahmad: (Anajifuta macho kwa kitambaa.) Sasa watakaje?

Rukia: Basi mtu si kupumzika!

Ahmad: Rukia huchoki na kunichungua. Ehe, habari gani zaidi?

Rukia: (Anainuka na kuanza kufutafuta vumbi mezani na juu ya viti.) Ile barua nishaipeleka.

Ahmad: Barua gani?

Rukia: Ile uliyowaandikia wazazi juzi.

Ahmad: Nilikuwa nimeshaisahau.

Rukia: Halafu ukishaisahau itakuwa vipi nawe ulikuwa wataka waje mwisho wa mwezi?

Ahmad: Bado kuna wakati.

Rukia: Naona wasahau kuwa barua yenyewe itachukua muda wa siku nne kuwafikia. Na leo ni tarehe ishirini, basi ikiwasili itakuwa imebaki juma moja tu.

Ahmad: Ah! Watakuja tu. (Anajitandaza kitini.) Mwezi ujao kutakuwa na sinema nzuri mjini.

Rukia: Tumalize habari ya wazazi kwanza. Kwani watakapokuja ni lazima tuwape pesa za kuwalipa wafanyakazi wa shambani na pesa zao za kujisaidia.

Ahmad: Habari hii tutaifanya taratibu taratibu nasi hatuwezi kujinyima starehe kidogo kwa sababu hiyo.

Rukia: Ndiyo, lakini ukumbuke kuwa hapo hapo mshaharani ndipo tutakapotoa kodi ya nyumba na matumizi ya kila siku.

Ahmad: Rukia sikuwezi.

Rukia: Huniwezi kwa sababu nakuonyesha ukweli?

Ahmad: Hayo tutazungumza baadaye. (Uk. 38-39).

Mwendo tritt ein.

Mwendo: Halima alikuwa hapa mchana.

Ahmad: (Anastaajabu.) Nani?

Rukia: Wajidai hukusikia?

Ahmad: Hebu ngoja kwanza. Ehe?

Mwendo: Halima amesema atakuja kesho jioni muonane.

Rukia: Mbona hukunieleza mimi?

Mwendo: Nilisahau. Pili, alipoondoka nilikwenda mjini.

Ahmad: Anitakia nini tena naye ndiye aliyenikimbia?

Rukia: Labda anataka mfanya suluhu, je?

Ahmad: Naona amechelewa basi (*Anainuka.*) Mwendo hebu njoo nikuonyeshe maua ninayotaka upalilie kesho.

Rukia: Sasa hivyo ni kusema utamngoja au vipi? Kumbuka kuwa kama amefunga safari kutoka nyumbani, ni lazima awe na neno muhimu.

Ahmad: (*Anaelekea mlango wa ndani.*) Waliosema kuwa “mchimba kaburi huingia mwenyewe¹⁰” kweli hawakukosa. (*Uk. 39-40*).

Halima ist für Ahmad kein Thema mehr.

2.2.11. Kitendo cha Nne. Onyesho la Pili.

Es ist Abend. Halima und Amina stehen vor einem kleinen Laden in Makupa bei Mombasa und warten auf einen Bus, der sie nach Changamwe bringen wird. Der Bus kommt nicht und Amina wird ungeduldig.

Sie kommen auf Sofia zu sprechen. Diese hat nämlich das Studium abgeschlossen und unterrichtet vorübergehend in einer Schule in Changamwe, unweit vom Hause Ahmads.

Amina: Na kama wewe ulisubiri sasa si ungekuwa kama yeye; nyumba nzuri, mshahara wa kutosha na staha mbele za watu?

Halima: Kijeraha kilichoanza kufanya kovu achana nacho, Mkasa?

Amina: Sina idhini kusema hivyo?

Halima: Idhini unayo kadiri utakayo. Lakini si kusubiri nikienda kupata mafunzo hayo?

Amina: Imekuwa mzazi hawezi tena kumwonyesha mtoto wake makosa?

Halima: (*Anaudhika.*) Hayo unaniuliza sasa! Si ninyi mlionipanga nisiendelee? Mkasema ati miaka miwili ni mingi?

Amina: Na hayo yote si tuliyaifanya ili mfunge ndoa na Ahmad?

Halima: Na yuko wapi huyo Ahmad sasa?

Amina: Yuko wapi vipi? Wajifanya hujui?

Halima: Najua sana aliko. Lakini hiyo ndoa mliyokuwa mkiikimbilia mbona mlivunja?

Amina: Na wamlaumu nani sasa?

Halima: Mimi sikukuuliza habari za lawama! Nataka kukuonyesha kuwa nyinyi ndio mlionaribu mambo kwa haraka zenu.

Amina: Si lazima ufanye kazi ndipo Abdalla akubali kukuoa. Ngoja kwanza tukamwone Ahmad. (*Uk. 42-43*).

Halima bezweifelt den Sinn der Reise. Amina meint zwar, daß Ahmad der Scheidung zustimmen werde. Halima macht Amina jedoch auf zwei Aussagen Ahmads aufmerksam:

Halima: Hakutwambia kuwa kujivuna kwetu kulikuwa mithali ya hasira za mkizi¹¹.

Amina: Ana nini hata kama alisema hivyo. Tunachotaka sisi ni akupe talaka basi!

Halima: Kumrudia tukimrudia kwaonyesha hasa akivyokwambia wewe, kuwa, “Mbio za sakafuni huisihia ukingoni.”¹² (*Uk. 43*).

10 Sprichwort

11 Sprichwort: Siehe „Dhamira Kuu“.

12 Sprichwort: “*Running on a roof ends at the edge*”. This proverb refers to flat roofs in areas with little rain. If it has no railing one is likely to topple over. Intentional meaning: *If you take too big a risk, you are in danger of ending badly.*

Halima macht sich Sorgen, denn wenn Ahmad ihr die Scheidung nicht gewährt¹³, kann sie Abdalla nicht heiraten und dann verliert ihr Vater bei ihm die Stelle.

2.2.12. Kitendo cha Nne. Onyesho la Tatu.

Einen Tag später um Mittag befindet sich Halima in Sofias Wohnung in Changamwe, Mombasa, die schön eingerichtet ist. Halima trägt immer noch die alten Kleider, die sie mitgenommen hatte, als sie Ahmads Haus verließ. Sofia, die einkaufen gegangen war, kommt zurück und ist überrascht, Halima in ihrem Haus zu finden. Sofia hatte Halima nämlich verraten, wie man das Haus auch ohne Schlüssel betreten kann. Sofia freut sich Halima zu sehen.

Sofia: (Anaketi juu ya kitanda.) Haya basi! Nipe habari za nyumbani.

Halima: Watu wote wa salama.

Sofia: Na huku ulikuja lini?

Halima: Nina siku mbili au tatu. (Uk. 46).

Halima teilt Sofia ihr Vorhaben mit. Sie ist mit ihrer mkasa Amina hergekommen. Sie möchten Ahmad besuchen.

Sofia: Na mlionana bila shaka.

Halima: Nilikuwa kwake jana jioni mimi na Mkasa Mjomba.

Sofia: Ehe.

Halima: Lakini alikuwa hajarudi kutoka kazini. Tuliyemkuta hapo ni Mwendo na msichana mmoja.

Sofia: Ni mkewe; aitwa Rukia. (Anamwangalia Halima kwa huruma.) Naam, ni mkewe huyo. Lakini ni msichana wa hapa hapa.

Halima: Alioa lini?

Sofia: Siku chache tu zilizopita. Lakini mkewe hakusoma sana labda mpaka darasa la saba hivi. (Kimya). Halafu ilikuwaje?

Halima: Muda mfupi baadaye alikuja, tukaingia faraghani.

Sofia: Ulikuwa na maneno ya siri nini?

Halima: Sikutaka huyo msichana asikie tuliyozungumza. Kwani ilikuwa habari ya talaka.

Sofia: (Anastuka.) Kwani anataka kukupa talaka?

Halima: Mimi ndiye nitakaye anipe talaka.

Sofia: Vipi tena Halima?

Halima: Maisha naye hayawezekani tena.

Sofia: Hayawezekani vipi?

Halima: Kwa kweli mimi sikumpenda Ahmad; bali nilikubali tufunge ndoa kwa vile baba na mama walitaka hivyo.

Sofia: Na basi baada ya kufunga ndoa naye vivyo hivyo kwa nini usivumilie?

Halima: Mambo mengi yalinifanya nirudi kwetu.

Sofia: Lakini mapenzi ni lazima wakati wote yawepo ndipo wawili waishi kama mume na mke. (Uk. 46-47).

Als Sofia Halima fragt, warum sie denn nicht gewartet habe, bis Kinder kommen,

13 Hanak, Irmi. 1996. „Language, Gender and Law: Divorce in the Context of Muslim Family Law in Zanzibar“, in: *Journal of African Cultural Studies*. London: SOAS. 9/1, S. 27-42. (Z.7.32.9/1.).

antwortet Halima, daß sie von Ahmad keine Kinder haben wollte, weil sie doch auf eine Ehe mit Abdalla gehofft hatte. Abdalla seinerseits verlangte, daß Halima noch zwei Jahre studiere, damit sie mit dem Lehramtspatent zum Familieneinkommen beitragen könne. Als Abdalla aber sah, daß Halima nicht einverstanden war, hat er sie vergessen und ihren Vater entlassen. Ahmad seinerseits hat Halima mitgeteilt, daß er ihr die Scheidung geben werde, wenn es ihm paßt.

Halima kennt sich nicht mehr aus. Auch finanziell geht es ihr schlecht.

Halima: (...) Basi nilikuwa naja kwako unipe msaada kidogo.

Sofia: (Anatabasamu.) Ni tayari kukusaidia kwa moyo wangu wote ikiwa naweza.

Halima: Nimepungukiwa na nauli ya kurudi nyumbani.

Sofia: Ni kiasi gani utakacho?

Halima: Mimi pamoja na mkasa mjomba itakuwa shilingi thelathini hivi.

Sofia: Ulikuwa na Mkasa Mjomba?

Halima: Naam.

Sofia: Si neno. (Anasimama.) Tende tukapike chai kwanza. Halafu nitakuangalia hizo pesa.

Sofia nimmt sich Halimas an.

Tamati